# NOBLE DECLARATION WITH SCRIPTURE

1. **Mimi ni mtoto wa Mungu**, nimeumbwa kwa mfano wake, nina utashi na akili nyingi, **ninakiri kuwa na nguvu na afya imara**.
   *Sawa na Neno linavyosema: "Basi Mungu akawaumba wanadamu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu aliwaumba; mwanamume na mwanamke aliwaumba."* – Mwanzo 1:27

2. Mimi ni **nuru**, kila ninapokaa **kutakuwa na nuru**.
   □ *Sawa na Neno linavyosema: "Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji uliojengwa juu ya mlima hauwezi kufichika."* – Mathayo 5:14

3. **Mwanga wangu utakua na nguvu**.
   □ *Sawa na Neno linavyosema: "Neno lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu."* – Zaburi 119:105

4. Mimi ni **chumvi**, kwa sababu yangu **wanaonizunguka watakuwa na ladha**.
   □ *Sawa na Neno linavyosema: "Ninyi ni chumvi ya dunia; lakini chumvi ikipoteza ladha yake, itakolezwa na nini? Haifai tena kwa neno lo lote, ila kutupwa nje, ikanyagwe na watu."* – Mathayo 5:13

5. Nimeumbwa kwa **kusudi**, **nitaliishi** na **kutitimiza kusudi**.
   □ *Sawa na Neno linavyosema: "Kabla sijakuumba katika tumbo la mama yako nalikujua, Na kabla hujatoka tumboni nalikutakasa; Nalikufanya kuwa nabii wa mataifa."* – Yeremia 1:5

6. Ninatamka **hatma yangu inalindwa na Mungu**, hakuna **uharibifu**, **upotevu**, wala **udanganyifu**.
   □ *Sawa na Neno linavyosema: "Maana atakuagizia malaika zake wakulinde katika njia zako zote."* – Zaburi 91:11

7. Nitaufikia **mwisho kwa utukufu** na **wakati sahihi**.
   □ *Sawa na Neno linavyosema: "Yeye aliyeanza kazi njema ndani yenu ataikamilisha hata siku ya Kristo Yesu."* – Wafilipi 1:6

NOBLE PARENTS DEPARTMENT

8. Nina akili sana, **ninaelewa darasani**.
 *Sawa na Neno linavyosema: "Moyo wa mwenye hekima hupata maarifa, Na sikio la mwenye busara hutafuta maarifa."* – Mithali 18:15

9. Nitakuwa **mkufunzi wa wakufunzi wangu**.
 *Sawa na Neno linavyosema: "Mwanafunzi hatampita mwalimu wake, lakini kila mtu akiwa mkamilifu atakuwa kama mwalimu wake."* – Luka 6:40

10. Nina **hekima sana**.
 *Sawa na Neno linavyosema: "Mwanzo wa hekima ni kumcha Bwana; Na kumjua Mtakatifu ni akili."* – Mithali 9:10

11. Mimi ni **mbeba majibu na masuluhisho yenye tija**.
 *Sawa na Neno linavyosema: "Maana Bwana huwapa hekima; Kinywa chake hutoka maarifa na ufahamu."* – Mithali 2:6

12. Nina **agano na Mungu**, mimi ni wake na yeye ni wangu.
 *Sawa na Neno linavyosema: "Nanyi mtakuwa watu wangu, nami nitakuwa Mungu wenu."* – Ezekieli 36:28

13. Mimi ni **udongo mzuri**, **hakuna mbegu mbaya itapandwa kwangu**.
 *Sawa na Neno linavyosema: "Na wengine wakaanguka penye udongo mzuri, wakazaa matunda, mmoja mia, mmoja sitini, mmoja thelathini."* – Mathayo 13:8

14. **Kila mbegu njema itakua na kumea**.
 *Sawa na Neno linavyosema: "Msidanganyike; Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna."* – Wagalatia 6:7

15. Mimi ni **baraka kwa watu**,
**Wanafunzi wenzangu**,
**Waalimu wangu**,
**Wazazi wangu**,
**Na kwa Mungu wangu**.
 *Sawa na Neno linavyosema: "Na nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka."* – Mwanzo 12:2

NOBLE PARENT'S DEPARTMENT

16. Ninajikabidhi **mikononi mwa Mungu**, na **kujisalimisha kuongozwa na Roho**.
    □ *Sawa na Neno linavyosema: "Na mwili wangu na nafsi yangu vimekufa njaa kwa Mungu aliye hai."* – Zaburi 84:2

17. **Yeye ndiye atakayeamua maisha yangu**.
    □ *Sawa na Neno linavyosema: "Bali tafuteni kwanza ufalme wa Mungu, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa."* – Mathayo 6:33

18. Najiungamanisha na **agano la msalaba na damu ya Yesu**.
    □ *Sawa na Neno linavyosema: "Lakini sasa, katika Kristo Yesu, ninyi mliokuwa mbali hapo kwanza mmekuwa karibu kwa damu ya Kristo."* – Waefeso 2:13

    *In Jesus' Name,*
    Mimi ni **mshindi**, na **siku yangu imebarikiwa**!
    □ *Sawa na Neno linavyosema: "Lakini katika mambo haya yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda."* – Warumi 8:37
    **In Jesus' Name, Amen!** □□

---

**Noble Parenting Department – Fountain Ministry**

**Noble Parenting** is a **faith-based department under Fountain Ministry**, dedicated to **equipping parents with biblical wisdom, parenting skills, and a strong foundation in Christ** to raise **Godly, responsible, and purpose-driven children** who will impact generations.

**Website:**www.fountainglobalministries.com
**Contact:** 0757052613 (WhatsApp)

NOBLE PARENTS DEPARTMENT